**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
**WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA**

# TANGAZO

## UUZAJI WA MITI YA MISAJI ILIYOPANDWA KWENYE MIPAKA YA MISITU YA HIFADHI KWA NJIA YA MNADA KATIKA WILAYA YA MUHEZA NA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILI NILO (KOROGWE)

1. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) unatarajia kuuza miti aina ya Misaji yenye jumla ya meta za ujazo **1,600.883** zilizopandwa kwenye mipaka ya misitu ya hifadhi katika Wilaya ya Muheza na Hifadhi ya Mazingira Asilia-NILO. Uuzaji huu utafanyika kwa njia ya mnada (Auction) kwa kuzingatia kifungu cha ya 31 (ii) cha kanuni za sheria ya Misitu za mwaka 2004. Mnada utafanyika tarehe 13 Agusti, 2019 katika ofisi ya Misitu Wilaya ya Tanga Saa Tano kamili (5.00) Asubuhi. Miti hii ya misaji itauzwa mahali ilipo na jinsi ilivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo.

2. Kampuni au mtu binafsi anayetaka kushiriki mauzo kwa njia ya mnada anatakiwa kuwasilisha maombi kwenye bahasha iliyofungwa kuonesha nia ya kushiriki mauzo kwa njia ya mnada akiambatanisha, usajili wa kiwanda cha kupasua magogo (Mwaka 2019/2020) na cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN). Aidha, anatakiwa aoneshe jina la msitu wa hifadhi, bei na ujazo anaotarajia kununua kwa kuzingatia miti iliyopandwa kwenye mipaka ya misitu ya hifadhi kama inavyobainishwa kwenye Jedwali Namba 1.

3. Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika ofisi ya Misitu Wilaya ya Tanga Mtaa wa Chumbageni jijini Tanga siku ya Jumanne **tarehe 13 Augusti, 2019** kwa kufuata sheria ya misitu Sura 323. Aidha miti iliyopandwa kwenye mpaka wa kila Msitu wa Hifadhi itanadiwa peke yake kulingana na bei na ujazo uliopo. Hata hivyo bei ya juu iliyotolewa na mnunuzi wakati wa kufungua bahasha haitazuia wanunuzi wengine kuongeza bei zaidi ya iliyotajwa awali. Mnunuzi atakayetoa bei ya juu atatakiwa kufanya

malipo kama ilivyoainishwa hapo chini kifungu namba 10. Baada ya malipo atasaini mkataba wa mauzo na Wakala wa kumruhusu kuvuna miti hiyo.

4. Wakala wa huduma za Misitu Tanzania unawaalika wanunuzi kutuma maombi yao kwa ajli ya kununua miti ya misaji kwa njia ya mnada ambapo mnunuzi anaweza kuchagua mojawapo kati ya mipaka ya misitu ya hifadhi yenye miti ya misaji kama ifuatavyo:

**Jedwali Na.1: Orodha ya Misitu ya hifadhi iliyopandwa miti ya misaji kwenye mipaka**

| Na | Jina la Msitu wa Hifadhi | Wilaya | LOT No. | Ujazo wa miti iliyopo kwenye mpaka wa msitu ($m^3$ ) | Bei pendekezi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kwani | Muheza | I | 602.89 | 415,000/= |
| 2 | Tongwe | Muheza | II | 631.20 | 415,000/= |
| 3 | Nilo NR | Korogwe | III | 366.793 | 450,000/= |
| | **Jumla** | | | **1,600.883** | |

5. Wakala wa huduma za misitu Tanzania utatoa hati ya ushindi kwa mnunuzi aliyetaja kiwango cha juu cha bei kwa kila ujazo wa miti ya misaji iliyopo kwenye mpaka wa misitu ya hifadhi katika jedwali Na.1.

6 Mnunuzi atakayefanikiwa kununua miti ya misaji hataruhusiwa kusafirisha magogo nje ya nchi isipokuwa baada ya kuchakata kwa mujibu wa kifungu cha 50 (1) cha kanuni za misitu za mwaka 2004 na Tangazo la Serikali Na.69 la Mwaka 2006.

7. Makampuni na watu binafsi wanakaribishwa kutembelea mipaka ya misitu yenye miti ya misaji wakati wa saa za kazi kuanzia saa mbili (2.00) asubuhi hadi saa tisa na nusu (9.30) alasiri isipokuwa siku za mapumziko. Meneja wa Misitu Wilaya ya Muheza au msaidizi wake atakuwepo kwa ajili ya maelekezo zaidi.

8. Wanunuzi wanapaswa kuchukua na kusoma masharti ya uvunaji wa miti ya misaji iliyopandwa kwenye mipaka ya misitu ya hifadhi ili kuepuka uharibifu wa misitu ya asili wakati wa uvunaji.

9. Kiwango cha juu cha bei kwa kila ujazo atakachotoa mteja kitajumuisha VAT, CESS, TaFF, Forest Royalty pamoja, na gharama za upandaji miti.

10. Mnunuzi atakayeshinda atalipa asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani yote ya ununuzi siku tatu (3) baadaa ya mnada kufanyika. Fedha hizo hazitarudishwa endapo mhusika atashindwa kukamilisha asilimia 75% iliyobaki ndani ya siku kumi na nne (14). Asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya mnada .Malipo yote yafanyike kwa kupitia mfumo wa makusanyo ya serikali (GePG) baada ya kupewa Bill. Hati ya madai inayoonesha kiasi cha kulipa itatolewa na meneja wa Misitu Wilaya ya Muheza na muhifadhi wa Mazingira Asilia-Nilo

11. Mnunuzi atapaswa kuwasilisha hati ya malipo kwa Meneja wa Misitu Wilaya ya Muheza kama uthibitisho wa malipo siyo zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.

12. Wanunuzi watakaoshinda watasaini mkataba na kupewa leseni ya kuvuna miti ya misaji na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ndani ya siku saba baada ya kukamilisha malipo ya gharama zote kwa asilimia 100% na atatakiwa kuondoa mazao yake katika kipindi cha mwezi mmoja baada ya kupewa leseni.

13. Maombi yote yawasilishwe siku ya mauzo kabla ya saa 4.30 asubuhi. Aidha wanunuzi watakaochelewa kuwasilisha maombi yao kwa siku na muda uliopangwa hawataruhusiwa kushiriki katika mnada.

14. Tangazo hili pia linaweza patikana katika tovuti zifuatazo www.tfs.go.tz na www.mnrt.go.tz]

**Imetolewa na:**

**MTENDAJI MKUU**
**WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA**


**S.L.P 40832**
**DAR ES SALAAM**
**SIMU NA.** : (+255) (022) 2864249
**NUKUSHI** : (+255) (022) 2864257
**BARUA PEPE**: mpingo@tfs.go.tz